***KISWAHILI Heart Book***

# MOYO WA BINADAMU



COPYRIGHT
ISBN 0 - 908367 - 34 - 1

E-MAIL: info@angp.co.za
**ALL NATIONS GOSPEL PUBLISHERS**
**P.0. BOX 2191, PRETORIA, 0001, R.S.A.**

(A Gospel Literature Mission financed by donations)
(Reg. No. 1961/001798/08)

Copyright: ANGP

## MOYO WA BINADAMU
## MAELEZO MAFUPI JUU YA KITABU HIKI

Kitabu hiki chenye vielelezo, kiliandikwa nchi ya Ufaransa mnamo mwaka 1732. Nacho kinajulikana kama "Kioo cha moyo cha kiroho" au "Kitabu cha Moyo". Kwa ajili ya kina kirefu cha ukweli, na thamani ya Maandiko Matakatifu yaliyomo, kitabu hiki kimetafsiriwa kwa karibu lugha zote za bara la Ulaya na kinasomwa na watu wa tabaka zote na imani zote.

Muhutasari wake, una mwelekeo wa mila fikra za kibantu. Kwa hiyo kinapendwa na kinasomwa na familia nyingi. Na wengi sana wameuona ukweli wa ahadi ya Mungu ilivyotolewa kwenye Agano la Kale na kutekelezwa katika Agano Jipya kama isemwavyo katika Ezekiel 36:26 na Waebrania 8:10 kuwa "Nitawapeni moyo mpya na kuweka roho mpya ndani yenu". Kwa hiyo wengi wenu mnaweza kuimba wimbo mpya mkisema: "Uliuawa, na kwa damu yako ulitukomboa na kuturudisha kwa Mungu, kutoka kwa kila kabila, watu wote na mataifa yote." Ufunuo 5:9.

Je wewe! Huwezi kujiunga katika maombi na kukitawanya kitabu hiki chenye msaada, "Kioo cha Moyo?"

J.R. Gschwend.

# MOYO WA BINADAMU

## Hekalu la Mungu au Kiwanda cha shetani? 1 Yohana 3:4-10.

Kwa Wasomaji:-

Kitabu hiki si kipya. Kilianza kuchapwa kwa mara ya kwanza katika nchi ya Ufaransa, yapata miaka mia mbili iliyopita. Kitabu hiki kimeletea watu elfu nyingi nuru na baraka kubwa. Kimetumiwa kama kioo cha roho ambacho wanaume na wanawake huweza kutumia na kujiona hali yao ya kiroho kama Mungu aiyonavyo. Wengi wameiyona mioyo yao yenye dhambi na kwa hiyo, wametubu na kupokea mioyo mipya na roho mpya katika kitabu hiki.

Usomapo kitabu hiki tafadhali ukumbuke ya kwamba ni kioo cha moyo ambacho waweza kusoma na kujitazama. Kama wewe u mmoja asiyeamini au Mkristo mwenye kurudi nyuma, utajiona hali yako kama Mungu aiyonavyo. Mungu hana upendeleo. Hutazama moyo wa mtu tu, bila kujali uso au rangi ya ngozi.

Shetani ni baba wa waongo wote, ni mkuu wa giza na ni mungu wa dunia hii. Hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru. Lakini, kwa kweli, yeye si malaika kama watu wengi wanavyomfananisha. Watu wa namna hii huchukizwa na picha imdhihirishayo shetani jinsi alivyo. Kama ilivyo kuwa katika siku za kale, vivyo hivyo hata siku hizi wako mitume wa uwongo, wafanyao kazi kwa hila na kujigeuza wawe mfano wa mitume ya Kristo. Hii si ajabu maana hata shetani mwenyewe hujigeuza na kuwa mfano wa malaika wa nuru. (2 Wakorintho 11:13-14). Shetani anawapofusha watu macho na fikara, ili wasiuwone upendo wa Mungu, wala utukufu na enzi ya Mungu na pia wasimuone Mkombozi wao, Yesu Kristo. (2 Wakorintho 4:4). Watu waliopofushwa macho na mungu wa dunia hii hawatambui ya kwamba wanakwenda mbio kwa nguvu, kukimbilia upotevu wa milele katika jehanum iwakayo moto. Mbele za Mungu wamekuwa wafu waliotawaliwa na mungu wa ulimwengu huu. (Waefeso 2:2).

Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa ili azivunje kazi za Ibilisi. (1 Yohana 3:8). Basi mtiini Mungu. Mpingeni shetani, naye atawakimbia. Mkaribishenii Mungu naye atawakaribisha. (Yakobo 4:7-8).

Usomapo kitabu hiki na kuzitazama picha zilizomo waweza kutazama moyo wako na kuuchunguza ili uwone hali yake ilivyo. Ukiona ya kwamba moyo wako ni mbaya na wenye dhambi, usifiche wala kukana, bali uridhike na kukubali kuziungama dhambi zako. Tukisema ya kwamba hatuna dhambi tunajidanganya wenyewe, wala kweli haimo mwetu lakini tukiziungama dhambi zetu Yeye ni mwaminifu na mwenye haki atatuondolea dhambi zetu na kutusafisha udhalimu wote. Tukisema ya kwamba hatuna dhambi tunamfanya Yeye kuwa ni mwongo wala Neno lake halimo ndani yetu. (1 Yohana 1:8-10). Basi, nyenyekeeni chiini ya mkono wa Mungu ili awasamehe dhambi zenu na kuwatakasa kwa damu ya Yesu Kristo yenye thamani kubwa.

Je, wewe unatawaliwa na Mungu au na shetani? U mtumwa wa dhambi au u mtumishi wa Mungu? Ikiwa dhambi hutawala maisha yako usikane bali umlilie Mungu, atakufanya kuwa huru katika Yesu Kristo aliye kuja ulimwenguni awaokoe wenye dhambi, awafumbue vipofu macho, atuondoe gizani na giza litoweke machoni petu. Alikuja ili atuweke katika nuru yake ya ajabu. Yesu alikuja kutufanya huru kutoka katika nguvu ya dhambi na ya shetani. Katika Yesu tumekombolewa kutoka katika dhambi zetu. Je, unasimama mbele za Mungu Mtakatifu aonaye na kujua siri zako zote, matendo yako yaliyofichwa na kila wazo lako? Huwezi kujificha, wala kuficha matendo yako kutoka usoni pa Mungu. Aliyetia sikio mahali pake, asisikie? Aliyefanya jicho asione? (Zaburi 94:9). Kwani macho yake ya juu ya njia ya mtu, naye huiyona mienendo yake yote. Hapana weusi wala hilo giza tupu, wawezapo kujificha watendao udhalimu. (Ayubu 34:21-22).. Kwa maana macho ya Bwana hukimbia-kimbia duniani pote, ili ajionyeshe kuwa

Copyright: ANGP

mwenye nguvu kwa ajili yao hao waliokamilika mioyo na kuelekea kwake. (2 Mambo ya Nyakati 16:9; Yohana 2:24).

Heri aliye samehewa dhambi na kusetiriwa makosa yake. Heri Bwana asiyemhesabia upotovu ambaye rohoni mwake hamna hila. (Zaburi 32:1-5 na Zaburi ya 51). Mpaka leo Yesu angali akiita: "Njoni kwangu ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. (Matayo 11:28-30).

## 1. PICHA YA KWANZA




Picha hii huonyesha moyo wa mtu asiyeamini na mwenye dhambi. Mtu huyu ni mwanaume au mwanamke wa ulimwengu huu aliyetawaliwa na mambo ya dunia hii na tamaa na juhudi ya mwili. Picha hii ni kioo cha kweli cha moyo wake kama Mungu amuonavyo. Macho yake yaliyo mekundu na yawashayo, huonyesha ulevi wake. (Mithali 23:29-32). Ni nani apigaye yowe? Ni nani aliye na macho mekundu? Ni wale wakaao sana kwenye mvinyo, waendao kutafuta divai iliyochanganyika. Utazame mvinyo mwekundu, uutiapo, blauri huchukua rangi yake, ishukapo taratibu. Mwisho wake huuma kama nyoka, huchoma kama fira. Macho yako yataona mambo mageni na moyo wako utatoa yaliyopotoka.

Chini ya kichwa waweza kuona moyo wa mtu. Moyo huu ni kikao cha wanyama mbalimbali, waonyeshao dhambi mbalimbali zilizomo moyoni mwa binadamu. Moyo ni kikao cha dhambi zetu. Mungu asema: "Moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote; una ugonjwa wa kufisha. Nani awezaye kuujua? (Yeremia 17:9).

©ANGP

Yesu mwenyewe alisema kuwa: "Kwa maana ndani ya mioyo ya watu hutoka mawazo mabaya, uasherati, wizi, uuaji, uzinzi, tamaa mbaya, ukorofi, hila, ufisadi, kijicho, matusi, kiburi na upumbavu. Haya yote yaliyo maovu yatoka ndani ya moyo, nayo humtia mtu unajisi. (Marko 7:21-23).

Tausi

Kiumbe cha kwanza ni tausi. Tausi ni ndege mzuri sana mwenye manyoya yenye rangi za ajabu. Hapa hufananishwa na dhambi ya kiburi. Nyota ya Alfajiri, kerubi mwenye kutiwa mafuta, aliyekuwa mchukuzi wa nuru kwa Mungu tena malaika wa Mungu, Ibilisi. (Isaya 14:9-17). (Ezekieli 28:12-17). Mwanzoni Ibilisi hakuwa malaika wa giza.

Kiburi hujionyesha katika njia nyingi. Baadhi ya watu hujivuna kwa ajili ya utajiri wao kama vile ng'ombe, kondoo, nyumba na mashamba, mavazi ya gharama kubwa,, uso mzuri na mwili ambao huuonyesha kwa aibu. Baadhi ya watu huwa na kiburi kwa sababu ya makabila yao, cheo kikubwa, elimu, nguvu, za mwili na kufanya matendo makuu katika ulimwengu huu, rangi ya ngozi na vitu vingi visivyo faa. Wengi hujaribu kujifanya kuwa wazuri kwa kuvaa bangili, vipuli na kujikata chale usoni na mwilini, ingawa Mungu aliumba mwili kamili. Mungu huwapinga wenve kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema. (1 Petro 5:5). Mungu huchukia kiburi na majivuno. (Mithali 8:13). Kiburi hutangulia uangamivu, na roho yenye kutakabari hutangulia maanguko. (Mithali 16:18).

Mbwa

Mbwa huonyesha tamaa za mwili, uovu, uasherati na zinaa. Kila aendako, mbwa hujitia unajisi. Watu wengi ni hali kadhalika kama mbwa; kila waendako huanza kuwabemba na kuwapendeza watu wengine, wanaume hata wanawake na kadha wa kadha. Uasherati na zinaa vinazidi kuwa vitu vibaya katika siku hizi za mwisho zenye uovu. Vijana wengi hawawezi kujizuia pia hata wanaume na wanawake walioa na kuolewa. Hata wajane wengi pia hukaa katika dunia ya uzinzi. Dhambi ya Sodoma pia imeshika uhai wa watu elfu nyingi, hata huyatimiza maneno ya Yesu ambayo aliyatabiri ya kwamba 'Siku za mwisho zitakuwa kama siku za Sodoma na Gomora. Wamaragoli na Wajaluo na makabila mengine humuita muasherati 'Mbwa'. Watu kama hao hawawezi kuurithi ufalme wa Mungu kwa sababu huko nje wako mbwa, wachawi, wazinzi, wauaji, waabuduo sanamu, na kila mtu apendaye uwongo na kuufanya. (Ufunuo 22:15). Kwa sababu hiyo, ikimbieni zinaa. Kila dhambi aitendayo mwanadamu ni nje ya wili wake, ila yeye afanyaye zinaa hutenda dhambi juu ya mwili wake mwenyewe. Hamjui ya kuwa ninyi ni hekalu la Mungu, yaani mwili wake? Mungu atamharibu mtu huyo kwa maana Hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ndilo ninyi.
(1 Wakorinto 3:16-18; 6:15-20).

Copyright: ANGP

Nguruwe

Nguruwe huonyesha dhambi ya ulevi na ulafi. Nguruwe hula chochote aonacho. Hachagui chema au kibaya. Hali kadhalika watu wengi hula nyama ya wanyama waliokufa wenyewe kwa ugonjwa au kupigwa. Hao hunywa damu na hula panya na mabuku ambayo Mungu alisema tusile. (Matendo 15:20; Isaya 66:17). Juu ya haya huifanyia unajisi miili yao ambayo ni hekalu la Mungu, kwa kutafuna na kuvuta tumbaku na sigara. Mambo haya hutia unajisi na kutia sumu damu yao kwa kuwaongoza katika mazoea ya dhambi. Shetani huwatawala kwa tamaa ya kuvuta. Ni kwa nguvu za Mungu tu, ya kuwa mwanamume na mwanamke yeyote aweza kuwekwa huru kutoka katika mazoea mabaya ya namna hii. Watu wengi, vijana hata wazee, hufikiri ya kwamba si kitu kulewa pombe au mvinyo. Walakini mlevi yeyote hawezi kuurithi Ufalme wa Mungu Pombe si chakula, bali ni kileo cha kifo ambacho huifadhaisha na kuibadili nia. Wale wanywao pombe huwa wapumbavu, hufanya uasherati na huuana. Wasipo tumia pombe hawawezi kufanya hivyo. Mvinyo hudhihaki, kileo huleta ugomvi, afanyaye makosa kwa ajili ya vitu hivi hana hekima. (Mithali 20:1). Chini ya sheria ya Musa yeyote aliyekuwa na mwana muasi tena aliyekuwa mlevi, mwana huyo alipaswa kupigwa mawe afe. (Kumbukumbu la Torati 21:1921). Wale wafanyao pombe ya namna yoyote ni wakosaji kama wale wanaokuza na

kunywa ile pombe kwa sababu Neno la Mungu husema: “Ole wao waliohodari wa kunywa kileo chenye nguvu, watu waume wenye nguvu huchanganya vileo.” (Isaya 5:22). “Ole wake yeye ampaye jirani yake kileo, wewe uitiaye sumu yako, na kumlevya pia.” (Habakuki 2:15). Msidanganyike; waasherati hawataurithi Ufalme wa Mungu, wala waabuduo sanamu, wala wazinzi, wala wafiraji, wala walawiti, wala waizi, wala watamanio, wala WALEVI, wala watukanaji, na wanyang’anyi. (1 Wakorintho 6:9-10).

Basi matendo ya mwili ni dhahiri. Nayo ndiyo haya uasherati, uchafu, uadui, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ULEVI, ULAFI, na mambo yanayo fanana na haya. Wao watendao mambo haya hawataurithi Ufalme wa Mungu. (Wagalatia 5:19-21). Tena msilewe mvinyo (tembo) ambayo ni ufisadi, bali mjazwe na Roho. (Waefeso 5:18). Yesu aliye chemchem ya uzima anawapa walio na kiu mwaliko huu: “Mtu akiona kiu, na aje kwangu anywe bure maji ya uzima.” (Yohana 7:37-38).

“Haya, kila aonaye kiu, njoni, majini,
Naye asiye na fedha: njoni nunueni mle;
Naam, njoni, nunueni divai na maziwa,
Bila fedha na bila thamani;
Kwani, kutoa fedha kwa ajili ya kitu ambacho si chakula?
Na mapato yenu kwa kitu kisichoshibisha? (Isaya 55:1-2).

Kobe

Mnyama huyu, ambaye hutembea pole pole, hufananishwa na dhambi ya uvivu, kukawia na uchawi. Yeye aliye mvivu huanguka katika majaribu mengi ya namna nyingi. Hupenda kuiba kuliko kufanya kazi. Wakati mwingine tendo hili la wizi humfanya hata atimize tendo la kuua ili apate kuiba. Uvivu wa roho hutuzuia tusiombe, tusisome Biblia na tena tusiende kanisani. Uvivu huu hutuzuia tusilichunguze Neno la Mungu ambalo lina uzima wa milele. Kukawia na kuchelewa ni mwizi wa wakati, kisha huongoza mpaka kwenye uharibifu. Mungu asemapo nawe ili umpe moyo wako leo, Ibilisi huja kwa mbio na hukuambia ukawie mpaka kesho au siku nyingine ambayo kamwe haitakuja. Labda utakawia siku kwa siku, mwaka kwa mwaka na mara ghafula kifo kitakufikia na utakufa bila kumjua Mungu, bila wokovu na bila Kristo. Kwa hiyo Mungu asema: “Leo kama mtaisikia sauti yake, msiifanye migumu mioyo yenu.” (Waebrania 3:7,8).

Gamba la mgongo wa kobe mara nyingi hutumiwa na waganga, kwa hiyo, hufananishwa na dhambi ya kuamini uganga na kufanya uchawi, badala ya kumuamini Mungu aliye hai. Badala ya kumuita Mungu aliye hai wakati wa ugonjwa na mateso, watu huamini sanamu, mizizi, mawe, pembe, au vitu vingine visivyo na uhai ambavyo vimependekezwa na mganga. Imewapasa kumuamini Muumba na Mwokozi wenu. Mungu aliwaamuru wana wa Israeli akasema: “Msimwache mwanamke mchawi aishi.” (Kutoka 22:18). Asionekane kwenu mtu atazamaye bao, wala mtu atazamaye nyakati mbaya, wala mwenye kubashiri wala msihiri. Kwa maana mtu atendaye haya ni chukizo kwa Bwana. (Kumbukumbu la Torati 18:10-12). Msiwaendee wenye pepo wala wachawi; msiwatafute ili wasimitie unajisi wao; Mimi ndimi Bwana Mungu wenu. (Mambo ya Walawi 19:31). Na mtu yule atakaye waendea wenye pepo na wachawi ili azini nao, nitakaza uso wangu juu ya mtu yule naye nitamtenga na watu wake. Jitakaseni basi, ili muwe watakatifu kwa kuwa Mimi ndimi Bwana Mungu wenu. (Mambo ya Walawi 20:6-7). Yesu Kristo ni Mpozi wa roho, na nafsi ya mwili. Yeye hutusamehe maovu yetu yote na kutuponya magonjwa yetu yote. (Zaburi 103:1-3). Kama mtu mmoja kati yenu hajiwezi kwa ajili ya homa na awaite wazee wa kanisa (si daktari) nao wamwombee na kule kuomba kwa imani kutamuokoa mgonjwa yule. Bwana atamuinua. Ikiwa amefanya dhambi,

Copyright: ANGP

atasamehewa. Ungamianeni dhambi zenu ninyi kwa ninyi na kuombeana ili mpate kuponywa. (Yakobo 5:14-16).

Usomapo kitabu hiki kidogo, kumbuka ya kwamba Mungu anasema na wewe na kukuambia utubu dhambi zako na kutoa maisha yako yote Kwake. Lakini moyo wako ulio na roho kama ya kobe hukunong'oneza na kukuambia, "Usiwe na haraka usijitoe leo, waweza kufanya hivyo kesho, au juma ijayo au mwaka ujao. Mshauri mumeo kwanza, mshauri mkeo au baba yako au watahiri watoto wako kwanza". Badala ya kutii sauti ya Mungu, unatii sauti ya udanganyifu ya Ibilisi. Kwa kufanya hivyo, waufanya moyo wako kuwa mgumu – hata huwa mgumu kama gamba la mgongo wa kobe.

Chui

Chui ni mnyama mkali sana aliye na hamu ya kumwaga damu. Hufanana na hasira na chuki na ghadhabu iliyo moyoni mwa mtu. Mtu yeyote anayetawaliwa na chuki na mwenye roho ya hasira, aweza kufanya au kuongozwa kufanya matendo ya ukatili, kulaani, kutukana na hata kuua. Mara nyingi imeonekana ya kwamba mtu alewapo pombe, hunywa roho ya Ibilisi, hata hawezi kujitawala mwenyewe. Waoga wengi hunywa mpaka wametosheka ili wapate ushujaa wa kutenda maovu au kutimiza kisasi kilicho moyoni. "Mvinyo wao ni sumu ya majoka, uchungu mkali wa nyoka." (Kumbukumbu la Torati 32:33). Kisasi ni kitamu kwa moyo wenye dhambi, bali Mungu ni mwenye kutoza kisasi. Yesu alisema: "Wapendeni adui zenu." Mungu aliahidi ya kwamba atazisamehe dhambi zetu kama tutawasamehe wanaotukosea.

Nyoka

Kiumbe hiki kilikuwa kizuri sana zamani; kiliwadanganya Adamu na Hawa katika bustani ya Edeni ili kuharibu ushirikiano wao na Mungu. Shetani aliona wivu alipoona jinsi Mungu alivyowapenda mwanaume na mwanamke wa kwanza. Tena aliona wivu walipowekwa kuwa watawala wa dunia badala ya Nyota ya Alfajiri, yaani Ibilisi. Kwa ajili ya wivu, shetani aliamua kuharibu ushirika uliokuwa kati ya Mungu na Binadamu. Alifaulu. Wivu huu wa kufisha umo moyoni mwako na unatawala maisha yako na tena hukunyima furaha wakati watu wengine wanapofurahi na kuishi vizuri. Hata Wakristo wamfanyiao Mungu kazi, inawapasa kujilinda na kujihadhari na roho ya wivu ya Ibilisi — hata Mungu akimtumia na kumbariki mtu mwingine kuliko wewe mwenyewe.

Wivu hutia moyo wako mawazo mengi ya uovu ili uwaloge wengine na kuharibu furaha yao na kuwaua wale unaoonea wivu na kijicho. Wivu ulio kati ya mume na mkewe waweza kuharibu unyumba wao na maisha yao. Wivu ni mkali kama ahera. (Wimbo Ulio Bora 8:6).

Chura

Chura hulia aridhini au majini. Anafanana na dhambi ya choyo au dhambi ya kupenda fedha na mali, ambayo ni shina la uovu wote. (1 Timotheo 6:10). Katika nchi ya Kongo kuna vyura wa aina fulani ambao hula mchwa mpaka wakapasuka na kufa. Mtu mwenye choyo hakubali kumgawia mwingine kilealichonacho au kuwapa maskini sehemu ya mali yake. Hujaribu kwa vyovyote, kwa haki au kwa uwongo, kukusanya mali za ulimwengu huu ambazo huharibika, huliwa na nondo, hushikwa na kutu na huibiwa na wezi. Bwana Yesu hutuambia tujiwekee hazina mbinguni kusiko na wezi wanaovunja na kuiba. Kwa maana hazina yako ilipo ndipo moyo wako ulipo. (Matayo 6:19-21). Akani na jamaa yake waliuawa kwa sababu walipenda dhahabu, fedha na mavazi ya thamani kubwa. Kwahiyo, akatwaa kile kilicho laaniwa. (Yosua 7).

Yuda Iskariote, mwanafunzi wa Yesu, alikufa kwa sababu ya kupenda fedha sana kuliko alivyokuwa akimpenda Bwana Yesu. (Matayo 27:3-5).

Copyright: ANGP

Shetani
Shetani ni baba wa waongo wote na wale wote wafanyao uwongo. Yeye ni mchungaji wa wanyama hao wote na mtawala wa mioyo yao. Yesu alisema: “Ninyi ni wa baba yenu Ibilisi na tamaa za baba yenu ndizo mzipendazo kuzitenda. Yeye alikuwa muaji tangu mwanzo, wala hana kweli ndani yake. Asemapo uwongo husema yaliyo yake mwenyewe kwa sababu yeye ni mwongo na ni baba wa uwongo.” (Yohana 8:44).

Nyota
Nyota hufananishwa na dhamiri iliyomo katika moyo wa kila mtu. Hapa dhamiri imekuwa nyeusi na kunajisika kwa ajili ya dhambi za mazoea ya uovu. Haiwezi kufanya kazi yake sawasawa. (1 Timotheo 4:2).

Jicho
Jicho la Mungu lipo mahali pote, tena huona chochote kilichomo ndani ya moyo wa mtu. Hakuna neno linalosetirika machoni pa Mungu. Kwahiyo Mungu huyajua na huyaona mawazo yote ya siri na makusudi ya moyo. Kama unafanya matendo yako maovu katika giza, mwituni au mahali popote, Mungu huona.

Malaika
Malaika hufananishwa na Neno la Mungu. Mungu anasema na mwenye dhambi aliyedanganyika na kumwambia atubu na airuhusu nuru ya Mungu iingie moyoni mwake. Mungu anasema na wewe, msomaji wa kitabu hiki pia.

Hua
Hua ni ndege ambaye hufugika na tena hadhuru mtu au kitu chochote. Ndege huyu ni mfano wa Roho Mtakatifu, Roho wa kweli ambaye huhakikisha dhambi, haki na hukumu. Katika picha Roho Mtakatifu yuko nje ya moyo; hawezi kukaa mahali ambapo dhambi inatawala.

Ndimi ndogo za moto
Ndimi hizi ambazo huzunguuka moyo wa mtu mwenye dhambi, zinafanana na upendo wa Mungu jinsi unavyo zunguuka moyo wa mtu mwenye dhambi. Mungu hataki mauti ya mwenye dhambi bali anataka atubu na kuishi. Yesu alikuja kuokoa wenye dhambi. Kutakuwa na furaha tele huko mbinguni kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye. Mungu ataka kuusafisha moyo wako kwa damu ya Mwanawe wa pekee, Yesu Kristo. Upendo wa Mungu hutaka uingie ndani ya moyo wenye baridi, uliokufa.

Yesu husimama mlangoni pa moyo wako na anabisha. Ukimfungulia ataingia na atausafisha moyo wako na atakuweka huru.

## 2. PICHA YA PILI

Picha hii inaonyesha mtu anayeanza kutubu na kumfuata Mungu. Malaika anashika upanga, yaani Neno la Mungu lenye uhai, lina nguvu na ukali kuliko upanga wowote ukatao kotekote. Neno la Mungu lina choma na huweza kuzigawanya nafsi na Roho na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake, tena lina wepesi kutambua mawazo na makusudi ya moyo. (Waebrania 4:12). Neno la Mungu linatukumbusha ya kwamba mshahara wa dhambi ni mauti. Mtu amewekewa afe mara moja na baada ya kufa ni hukumu. (Waebrania 9:27).



Copyright: ANGP

Fungu la mwenye dhambi na yeye asiye amini litakuwamo katika ziwa liwakalo moto kwa kiberiti.





Katika mkono wa pili, malaika ameshika fuvu la kichwa, yaani mifupa mikavu ya kichwa. Jambo hili humkumbusha mwenye dhambi ya kwamba sisi sote imetupasa kufa. Haidhuru ingawa twaipenda sana miili yetu hata tunaihifadhi na nguo na kula vyakula na kuridhisha tamaa zake, lakini itakufa na kuoza. Mabuu watakula mwili wakati roho itakapodhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu. Mwenye dhambi aanza kusikia Neno la Mungu linaloonya na hufungua moyo wake kwa upendo wa Mungu. Roho Mtakatifu aanza kung'aa ndani ya moyo wenye giza. Nuru ya Mungu yaingia na kuanza kufukuza giza lote. Mahali penye mwangaza, giza hukimbia. Upendo mwema wa Mungu umeamsha moyo wa baridi. Dhambi iliyofananishwa na wanyama mbalimbali imelazimishwa kukimbia.

Ewe mwenyi dhambi, mkubali Yesu aliye nuru ya ulimwengu aingie moyoni mwako. Akisha ingia, giza pamoja na matendo ya giza yataondoka katika moyo wako. Kama unavyoona katika picha hii. Yesu asema, "Mimi ndimi nuru ya ulimwengu, yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe." (Yohana 8:12)

. Ole wao wanaopenda giza kuliko nuru. Yesu alipoingia katika hekalu kule Yerusalemu aliwafukuza wote waliokuwa wakiuza ng'ombe, kondoo na njiwa. Akamwaga fedha za wale waliokuwa wakibadilisha fedha kisha akasema, "Nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala, bali ninyi mmeifanya pango la wanyang'anyi." (Matayo 21:12-13). Nyumba ni moyo wako. Yesu hakuja ili azisamehe dhambi zetu tu, bali alikuja kutukomboa na kutuweka huru kutoka katika nguvu ya dhambi na utawala wa dhambi. Basi, Mwana akiwaweka huru, mtakuwa huru kweli kweli. (Yohana 8:36).

## 3. PICHA YA TATU





Katika picha hii twaona moyo wa mwenye dhambi aliyetubu kweli. Anasikia na kuona ukubwa na uzito wa dhambi zake nyingi, ambazo, kwa sababu ya hizo dhambi, Yesu alisulibishwa msalabani. Moyo wa mwenye dhambi huvunjika utazamapo msalaba ambao malaika, yaani Neno la Mungu, humfunulia. Upendo wa Mungu ulioonekana katika Yesu Kristo wasikitisha moyo wake, hasa akumbukapo ya kwamba Yesu Kristo, Mwana Kondoo wa Mungu, alikuja kuziondoa dhambi zake zilizo nyingi. Akakubali afe msalabani badala yake. Ni jambo la kweli kuwa Yesu alipigwa mijeledi, alivikwa taji la miba, alipigiliwa misumari mikononi na miguuni, aliangikwa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu. Jamo hili ndilo linalovunja moyo wake yeye mwenye dhambi aliyetubu. Asomapo Neno la Mungu na kulifahamu hujiona katika kioo cha Mungu; hufahamu jinsi moyo wake ulivyo katika giza la dhambi. Moyo wake huchomwa na roho yenye majuto. Huzuni humfanya alie kwa ajili ya dhambi zake na Mungu humkaribia. Upendo wa Mungu na amani yake huingia katika moyo wake uliotakaswa na damu yake Yesu Kristo ili dhambi zake zote ziondolewe.

Aanza kufahamu ya kwamba Bwana yuko karibu nao waliovunjika mioyo, na waliopondeka roho, huwaokoa. (Zaburi 34:18). Huwaponya waliopondeka mioyo na huzitibu jeraha zao. (Zaburi 147:3). Tena Neno la Mungu husema, “Mtu huyu ndiye nitakayemwangalia, mtu mwenye roho iliyopondeka, atetemekaye asikiapo Neno langu. (Isaya 66:2).

Roho Mtakatifu na upendo wa Mungu hutawala moyo uliosafishwa. Anapoutazama msalaba kwa imani, na anapoitazama damu ya Yesu, iliyomwagika kwa ajili ya kuziondoa dhambi zetu, mtu huyu anaanza kufahamu ya kwamba dhambi zake zimesamehewa. Sasa anapata uhakika moyoni mwake ya kwamba damu yake Yesu, Mwana wa Mungu, imesafisha dhambi zake zote. (1 Yohana 1:7). Yeye amuaminiye Yesu hata potea, bali huwa na uzima wa milele. (1 Wakorintho 6:10,11). Katika Yesu tunao ukombozi wa damu yake, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake. (Waefeso 1:7). Sasa ana roho mpya moyoni mwake, na kutoka hapa, haupendi ulimwengu huu wala vitu vya dunia hii, bali hutamani vitu vya Mungu, ambaye amemjazia moyo wake upendo Wanyama, yaani dhambi zake, wako nje ya moyo wake, ijapokuwa shetani mwenyewe hapendi kwenda, tena angali akitazama nyuma na anatamani

kuingia moyoni tena. Kwahiyo, tumeambiwa tukeshe na kuomba, tena tumpinge shetani, naye atatukimbia.

## 4. PICHA YA NNE




Picha hii inafanana na Mkristo aliyepata amani na ukombozi kamili katika dhabihu ya Bwana wetu na Mkombozi, Yesu Kristo. Kwa hiyo, haonei fahari kitu chochote ila msalaba wa Yesu Kristo, ambao kwa huo, ulimwengu umesulibishwa kwake, na Yeye kwa ulimwengu. (Wagalatia 6:14). Anafahamu kabisa ya kwamba Yesu alikufa msalabani ili sisi tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki. (1 Petro 2:24). Mkristo husulibishwa na ulimwengu huu. Tumeagizwa tuiendee roho wala tusitimize kamwe tamaa za mwili (Wagalatia 5:13-25). Tena tumeambiwa tutafute kwa bidii utakatifu, ambao bila huo hakuna atakaye mwona Bwana. (Waebrania 12:4).

Katika picha yenye moyo huu waweza kuona nguzo ambazo Yesu alifungwa na pingu baada ya kuvuliwa nguo zake. Waweza kuiyona mijeledi ambayo waliitumia kumpigia, kwa ajili ya adhabu ambayo ilipasa kutuangukia sisi, lakini ilimuangukia yeye. (Isaya 53:11,12). Alipigwa kwa ajili ya dhambi zetu. Mfalme Herode na watu wake walimdhihaki na baada ya kumpiga

Yesu mijeledi, wakamvika vazi jekundu. Wakasokota taji la miba na kumvika kichwani badala ya kumvika taji la dhahabu. Wakaweka mwanzi katika mkono wake wa kuume badala ya kuweka fimbo ya kifalme. Wakapiga magoti mbele yake na kumdhihaki wakisema, Salamu, mfalme wa Wayahudi! Kisha wakamtemea mate, wakatwaa ule mwanzi, wakimpiga–piga kichwani. Walipokwisha kumdhihaki walimchukua ili asulibishwe. Wako wengi waitwao Wakristo na huenda kanisani, huhudhuria meza ya Bwana, humwimbia Mungu nyimbo, lakini matendo yao maovu humsulibisha tena Mwokozi wao. Si wote waombao na kusema Bwana, Bwana, watakaoingia katika ufalme wa Mungu, bali ni wao wafanyao mapenzi ya Baba yao aliye mbinguni. (Matayo 7:21-27). Katika picha waweza kuona mfuko wa fedha. Yuda alimsaliti Yesu akamuuza kwa vipande thelathini vya fedha, kwa sababu upendo wa fedha ulimpofusha na ulitawala moyo wake. Taa, na minyororo na kadhalika vilitumiwa na askari walipopigia kura


mavazi Yake ili kutimiza Neno la Mungu lililobashiriwa zamani. “Wanagawanya nguo zangu, na vazi langu wanalipigia kura.” (Zaburi 22:18).

Mara askari alipomchoma mkuki wa ubavuni, damu na maji vilitoka. (Yohana 19:33-37). Kabla jogoo hajawika, Petro alimkana Yesu mbele ya kijakazi. Je, unamkiri Yesu kwa maneno na matendo? Ama unaogopa kufanya hivyo? Yesu alisema, “Basi, kila mtu atakayenikana mbele ya watu, nami nitamkana mbele ya Baba yangu aliye mbinguni.” (Matayo 10:32,33). Tena alisema, “Mtu yeyote akitaka kunifuata ni lazima ajikane nafsi yake na ajitwike msalaba wake na kunifuata. (Matayo 16:24). Wala mtu asiyechukua msalaba wake akinifuata, hanistahili. (Matayo 10:33).

Mwamba ulio imara, Kwako nitajificha, Maji hayo na damu, Yaliyotoka humu,
Hunisafisha dhambi, Hunifanya mshindi.

ANGP

## 5. PICHA YA TANO




Katika picha hii twaonyeshwa maisha yaliyotakaswa, na mwenye dhambi aliyeokoka kwa ajili ya neema na rehema za Mungu amekuwa hekalu la kweli la Mungu, makao ya Mungu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu; kama alivyosema Bwana Yesu, “Mtu akinipenda atalishika Neno langu na Baba yangu atampenda, nasi tutakuja kwake na kufanya makao kwake.” (Yohana 14:23). Katika Yesu Kristo Mungu amemheshimu mtu tena amembariki na kumkweza. (Luka 1:52).

Sasa moyo umekuwa hekalu la Mungu aliye hai. Dhambi imeondolewa. Badala ya wanyama mbali mbali waliotawaliwa na shetani, baba wa uwongo, tunaona Roho Mtakatifu hukaa moyoni. Badala ya matendo maovu ya mwili umekuwa kama shamba lenye mazao au mti uzaao matunda. Huzaa matunda ya Kiroho kama: Upendo, furaha, amani, unyenyekevu, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, na matunda mengine yampendezayo Mungu na binadamu.

Mwenye moyo huu amekuwa tawi la kweli; huzaa matunda katika mzabibu wa kweli, yaani Yesu Kristo, Bwana wetu. Siri ya kuzaa matunda ni kuwa mtu akaaye ndani ya Kristo na Kristo

hukaa ndani yake. (Yohana 15:1-10). Tena huweka Neno la Mungu moyoni mwake kwa sababu hujazwa na kubatizwa na Roho Mtakatifu aliye na nguvu kuushinda mwili na tamaa zake. Kwa nguvu za Roho Mtakatifu aweza kwenda katika Roho. Haishi tena kwa vile ambavyo huviona au huvisikia bali huishi kwa amani, kwa kuwa ana imani katika Yesu: Huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu. Huishi kwa tumani na huimarishwa kwa tumaini la kuja kwake, Bwana wetu Yesu Kristo. Huishi katika upendo wake Mungu ambao huhudumu milele.

Heri walio na mioyo safi, maana hao watamwona Mungu. (Matayo 5:8). Ingawa Mfalme Daudi alikuwa tajiri, aliwashinda adui zake, na akamuua Goliati na wengine, lakini alikuwa na haja moja kubwa. Kwa moyo alilia: “Ee Mungu, uniumbie moyo safi, uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu.” (Zaburi 51:10). Hakuna mtu awezaye kujisafisha moyo wake wala kujiumbia moyo mpya. Imempasa amjie Mungu kwa unyenyekevu na kuziacha dhambi zake kama Mfalme Daudi alivyofanya. Imempasa awe kama mwana mpotevu, aliyewaacha nguruwe na akarudi kwa baba yake na akasema, “Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako.” Mungu yuko tayari kumsaidia kila mwenye dhambi amjiaye kwa roho ya unyenyekevu. Mungu alisema, “Nami nitakupa moyo mpya, Nami nitatia roho mpya ndani yako, Nami nitauondoa moyo ulio kama jiwe katika mwili wako, Nami nitatia Roho yangu ndani yako, ili uende katika amri zangu.” (Hili ndilo Agano Jipya ambalo Mungu alilifanya na kulitia mhuri kwa damu ya Mwanawe, Yesu Kristo.


Katika picha hii ya tano twaona malaika akitokea tena, na kuwahudumia wale ambao watairithi ufalme wa uzima wa milele. Tena huwazunguukia wamchao Bwana. (Zaburi 34:7; 91:11; Danieli 6:22; Matayo 2:13,19; 18:10; Matendo 5:19; 12:7-10). Pia shetani huonekana katika picha hii, akisimama karibu na moyo na kutafuta nafasi ya kurudi tena katika makao yake ya zamani. Kwa hiyo twaambiwa, “Muwe na kiasi na kukesha, kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguuka zunguka, akitafuta watu awameze.” (1 Petro 5:8). Mpingeni shetani naye atawakimbia. (Yakobo 4:7).

Copyright: ANGP

## 6. PICHA YA SITA

Picha hii inayotia huzuni ni picha ya mtu mwenye kurudi nyuma. Jicho lake moja limeanza kufunga. Yaonyesha ya kwamba mtu huyu anaanza kuwa baridi na kushikwa na usingizi katika maisha yake ya Kikristo. Jicho lake lingine, kwa aibu, hutazama mahali pote, ili ajaribu kuupendeza ulimwengu. Nuru iliyokuwa moyoni mwake imeanza kuzimika. Hataki tena kuteswa pamoja na Kristo. Sasa amekuwa katikati ya majaribu na ameanza kuyakubali kuliko kumpinga shetani. Anachagua kumsikia shetani kuliko Mungu. Ijapokuwa angali akihudhuria mikutano ya Kanisa na hujaribu kuficha ya kwamba anaupenda ulimwengu, ulio moyoni mwake, sasa analegea na humkimbia Mungu. Amepoteza upendo wake wa kwanza kwa Mungu. Nyota ya moyoni mwake, yaani dhamiri, imezimika na msalaba umekuwa mzigo mzito kwake. Imani yake inaanza kuwa haba na anakoma kushirikiana na Mungu katika kuomba. Amekuwa mvivu kwa hali ya moyo, na humpa shetani nafasi.

Roho ya Tausi yatafuta mahali pa kuingilia. Mwenye kurudi nyuma amekuwa mwenye kiburi na amesahau ya kwamba aliokoka kwa ajili ya neema peke yake. Ulevi pia unabisha katika moyo wake, unatafuta mahali pa kuingilia. Labda mtu fulani humshawishi anywe pombe. Anamwambia, “Haidhuru, kunywa kidogo tu,” Hafahamu ya kwamba kunywa pombe kidogo tu, ni kama kijito ambacho huongoza mpaka kwenye jito la ulevi. Pengine mwanamke fulani humtengenezea Bwana wake na rafiki zake pombe na huyu mwanamke hujiridhisha mwenyewe na husema ya kwamba yeye mwenywe hanywi pombe lakini amesahau ya kwamba yeye huwafanya wengine wanywe pombe tena anadanganywa na roho ya ulevi na uasherati. Hupenda kutembea pamoja na rafiki waovu na kwenda mahali penye anasa. Labda fulani humwambia ya kwamba kucheza ngoma kama Wazungu wanavyofanya si dhambi, lakini kucheza ngoma kama wale




waliostarabika, Wazungu, ni dhambi. Hujui ya kwamba mahali popote pa kuchezea ngoma huvuta watu wafanye dhambi? Kuvuta sigara zipatikanazo madukani ni vibaya kama kuvuta tumbaku lipatikanalo nyumbani. Yesu, kamwe, hakuvuta sigara wala Mkristo aliyemfuata.

Shetani amwambia kwamba si kitu kufanya dhambi mara ya kwanza au kuzini mara moja tu. Shetani akimwambia haya hata pepo wa uasherati hupata mahali pa kuingilia katika moyo wake uliosafishwa, na anaushika tena.

Mtu aonekanaye katika picha achomaye moyo kwa kisu anafanana na wale wanaodhihaki Ukristo kwa maneno na machongezi. Mwenye moyo hawezi kuvumilia zihaka za watu, hasa rafiki zake. Maneno yao huchoma moyo wake, na tangu upendo wa Mungu umepoa, yeye huanza kuwaogopa watu kuliko Mungu. Tena kwa sababu ya hofu juu ya fikara za watu, yeye amekuwa mtumwa wa binadamu na amerudi nyuma.

Copyright ANGP

Ghadhabu na chuki vimetokea tena; mateso na taabu hutawala moyo wake. Matusi yametia unajisi midomo ambayo aliitumia kumsifu Mungu na kumwomba. Ikiwa Ibilisi aweza kupata kipenyo au mlango mdogo, ataingia, tena atapanua kipenyo ili dhambi nyingine ziingie.

Ni rahisi kuruhusu dhambi ya kupenda fedha iingie moyoni tusipo yajali maonyo ya Bwana Yesu yanayosema, "Kesheni, mwombe, msije mkaingia majaribuni." (Matayo 26:41). Anayejidhani ya kwamba amesimama na aangalie asije akaanguka. (1 Wakorintho 10:12). Basi, imetupasa kuvaa silaha zetu za Kimungu, ili tupate kuweza kuzipinga hila za shetani. (Waefeso 6:18).

## 7. PICHA YA SABA

Picha hii yaonyesha hali ya moyo wa mtu aliyerudi nyuma, kwa kuwa baada ya kupewa nuru na kukionja kipawa cha mbinguni, na kufanywa msharika wa Roho Mtakatifu, ameanguka. Tena picha hii yaonyesha hali ya mtu asiyetubu. Ingawa amehubiriwa Injili na imefunuliwa machoni pake, lakini huufanya moyo wake mgumu, na huendelea kufanya dhambi.

Yesu mwenyewe alieleza hali ya mtu mwenye kurudi nyuma aliposema, "Pepo mchafu amtokapo mtu, hupitia mahali pasipo na maji akitafuta mahali pa kupumzikia; asipopaona

husema nitairudia nyumba yangu niliyoitoka hata afikapo, akaiona imefagiwa na kupambwa. Ndipo huenda akachukua pepo wengine saba walio waovu kuliko yeye mwenyewe, wakaingia na kukaa humo na mtu yule hali yake ya mwisho huwa mbaya sana kuliko ya kwanza." (Luka 11:24-27). Yaliyomtukia mtu huyu ni sawasawa na ile Mithali ya kweli isemayo, "Mbwa ameyarudia matapishi yake mwenyewe, na nguruwe aliyeoshwa amerudia kugaa-gaa matopeni."



Maandiko haya yaidhihirisha hali ya moyo wa mtu huyu. Dhambi, kwa ajili ya hila zake zote, imekuja kukaa moyoni na kutawala. Hata uso wake waonyesha jinsi moyo wake ulivyo haribika. Imempasa Roho Mtakatifu aondoke moyoni kwa sababu dhambi na Roho Mtakatifu hawawezi kukaa pamoja. Nuru haina ushirikiano na giza. Moyo hauwezi kuwa hekalu la Mungu na tena uwe pango la shetani. Imempasa malaika, yaani Neno la Mungu, aondoke kwa huzuni huku anatazama nyuma akitumaini ya kwamba mwenye moyo atatubu tena kama Mwana Mpotevu alivyofanya. Mwana mpotevu alijuta moyoni mwake alipokuwa akikaa katikati ya nguruwe na kula masazo ya chakula kilicholiwa na nguruwe, wala hakuna mtu aliyempa chochote. Akafahamu hali yake ya kurudi nyuma na upotevu wake. Akatubu, akisema, "Nitaondoka, nitakwenda kwa baba yangu na kumwambia, 'Baba nimekosa juu ya mbingu na mbele yako, sistahili kuitwa mwanao tena'." Kwa sababu ya toba yake ya kweli na huzuni juu ya dhambi zake, baba yake alimsamehe, akamfanyia sikukuu na kumchinjia ndama.


Lakini katika mfano wa picha hii, mtu huyu hana roho ya toba ya kumsaidia arudi kwa Mungu, wala kuanguka miguuni pa Yesu, wala kumsihi ili apate masamaha na utakaso. Dhamiri yake imechomwa moto, ikafa. Anayo masikio lakini hawezi kusikia sauti ya Mungu tena. Anayo macho lakini hawezi kuliona shimo la kuzimu ambamo yu karibu kujitupa. Hana aibu tena, wala toba. Huendelea kufanya dhambi zake kwa wazi. Shetani amekuja kutawala moyo wake na anakaa katika kiti chake cha enzi kama mfalme. Labda kwa nje mtu huyu angali akijisifu kwa ajili ya kuonekana kuwa mzuri, kama makaburi yaliyopakwa chokaa ambayo kwa nje huonekana kuwa mazuri kumbe ndani yamejaa mifupa ya wafu na uchafu wa dhambi. (Matayo 23:27). Baba wa uwongo amechukua mahali pa roho ya kweli. Kila mnyama, yaani kila dhambi, anaye pepo wake mchafu amsaidiaye kutawala moyo. Ijapo kuwa angependa kujiweka huru kutoka kwa watesi wachafu, lakini hawezi kwa sababu amekuwa mtumwa wao. Sasa anapata hakika ya yale ambayo Mungu aliyasema kwa Mtume Petro: "Mwaonaje? Haikumpasa adhabu iliyo kubwa zaidi mtu yule aliyemkanyaga Mwana wa Mungu, na kuihesabu damu ya Mwana wa

COPY - ANGP

Mungu kuwa kitu cha ovyo, na kumfanyia jeuri Roho wa neema?" (Waebrania 10:29-31; 2 Petro 2:1-14).

Msomaji mpenzi, ikiwa moyo wako una hali ya namna hii, mlilie Mungu kwa moyo wako wote. Yeye huweza, tena anapenda, akuokoe na kukusamehe dhambi zako zote na kukutakasa, kama ukimjia na kutubu kwa roho ya kweli. Pia huweza kumfunga Ibilisi pamoja na jeshi lake na kumtupa nje kutoka katika moyo wako, kama ukipenda afanye hivyo. Umjie Bwana kama yule mwenye ukoma alivyomwendea Yesu akalia, "Ukitaka waweza kunitakasa," na Yesu akasema, "Nataka, takasika." (Marko 1:40-43). Lakini ukiendelea kuufanya moyo wako mgumu, tena ukipenda giza kuliko nuru, hakuna tumaini wala msaada kwa wewe, kwa sababu unachagua mauti badala ya uzima, giza badala ya nuru.

## 8. PICHA YA NANE




Katika picha hii twaona mwenye dhambi aliye na moyo ngumu, tena aliyerudi nyuma. Mwili wake umejaa hofu ya mauti. Mauti, yaani kifo, amekuja wakati asioutazamia wala kuutumaini. Anasa za dhambi zimetoweka na mshahara wa dhambi unapaswa kulipwa. Maumivu ya jehanum yanaishika roho yake, yenye kutishwa. Ijapokuwa anataka kuomba, anaona ya kwamba hawezi kushirikiana na Mungu. Maneno yote ya rafiki zake wa dunia hii hayawezi kumsaidia kwa sababu hayafai kumfariji. Tena hawezi kujiokoa kwa mali zake ambazo alizikusanya kwa ajili ya kupenda fedha. Wala haziwezi kuyatuliza maumivu yake, wala kuongeza umri wake. Ijapokuwa anajaribu kumfikiri Mungu, shetani hampi nafasi yoyote. Kila kitu anachokipenda humu duniani kinaonekana ya kwamba kinamdhihaki hata viongozi wake wa uwongo hawawezi kumsaidia. Aanza kufahamu ya kwamba ni jambo la kutisha, kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai. Alikuwa akitumaini kupata haki mbele za Mungu alipopata ugonjwa wa kufa, lakini sasa aona ya kwamba amechelewa.


ANGP

Watu wengi wamekufa ghafla bila kupata nafasi ya kumtafuta Mungu, walipopatqa ugonjwa wa kufa. Kwa hiyo, twaambiwa tumtafute Bwana, maadamu anapatikana. Badala ya kusikia Neno la msaada la Bwana, huyu mwenye dhambi anayekufa, ambaye alikataa neema ya Mungu na

upendo wa Mungu, katika maisha yake, inampasa kusikia sauti ya hakimu wake isemayo, “Ondoka kwangu, uliye laaniwa, nenda katika moto wa milele, uliowekwa tayari kwa Ibilisi na malaika zake.” (Matayo 25:41). Mtu amewekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu. (Waebrania 9:27).

Dhahiri, ndihyo haya, Uasherati, Uchafu,
Ufisadi, Ibada ya sanamu, Uchawi, Uadui,
Ugomvi, Wivu, Hasira, Fitina, Faraka, Uzushi, Husuda, Ulevi Ulafi.
Gal. 5:19-21

## 9. PICHA YA TISA




Katika picha hii twaona Mkristo wa kweli anayestahimili na kushinda majaribu makali ya mwili na ya Ibilisi. Hujaribiwa pande zote, bali yeye hustahimili mpaka mwisho. Katika Yesu Kristo ameshinda mengi zaidi na hakuanza mashindano ya Ukristo tu, bali huyatimiza mashindano haya pia kwa kumtazama Yesu, Mwenye kuanzisha na Mwenye kutimiza imani yetu. (Waebrania 12:1,2).

Shetani pamoja na jeshi lake hutembelea moyo wenye kuamini na hujaribu kupata mahali pa kuingilia, bali ni bure, hafanikiwi. Kiburi na upendo wa fedha, na roho ya uasherati vinabisha.

Badala ya mbwa na chui twaona ‘beberu na punda’ kwa sababu mara kwa mara dhambi hujigeuza kuwa mfano mwingine au kujiita kwa jina lingine. Bali Mkristo anayekesha huona dhambi katika kila mfano, hata dhambi ingemjia katika jina la dini au kama malaika wa nuru. Kwa sababu Neno la Mungu na Roho ya kweli iliyomo moyoni mwake, humwongoza katika kweli yote, tena humsaidia kutambua mema na mabaya.

ANGP

Karibu ya wanyama na pepo wabaya, waweza kuona mtu akicheza ngoma mbele ya Mkristo anayestahimili; mtu huyu ameshika kikombe cha divai au pombe, mkononi mwake. Anamjaribu Mkristo kwa anasa za ulimwengu huu, na kwa kileo cha kucheza ngoma, lakini dhambi hizi haziwezi kumsikitisha Mkristo aliyewekwa wakfu na aliyeacha dhambi na anasa za uimwengu. Kwa ajili ya mambo haya, amemkaribia Mungu. Mtu mwingine anamchoma kisu. Haya yote yanachoma moyo wake, matusi, masingizio, dhihaka na vitisho vyote humjia kutoka kwa wasioamini na waitwao Wakristo kwa jina tu. Bali yeye Mkristo anayestahimili hujifariji kwa maneno ya Yesu yasemayo, “Heri ninyi watakapowashutumu na kuwaudhi na kuwanenea kila

neno baya kwa uwongo, kwa ajili yangu. Furahini na kushangilia kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa mbinguni. (Matayo 5:11,12).

Dhambi, na mwili ambao ni MWENYEWE, na Ibilisi, wana jaribu kwa bidii kuwatenga Wakristo na upendo wa Mungu. Bali kwa ujasiri wa Wakristo wanaostahimili husema, "Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo Je! Ni dhiki, au shida, au adha, au njaa, au uchi, au hatari, au upanga? Lakini katika mambo haya yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda." (Warumi 8:35-39).
Kwa kuvaa silaha zote za Mungu, Mkristo anayestahimili aweza kusimama imara katika siku za majaribu na kwa nguvu za Roho Mtakatifu hushinda mwili na majaribu mengine yote. Hufahamu ya kwamba Kristo, akikaa moyoni mwake Yu wenye nguvu kuliko Ibilisi na jeshi lake, kwa sababu Yeye aliye ndani yetu ana nguvu nyingi zaidi kuliko yule aliye ulimwenguni, yaani shetani. Yesu Kristo alimshinda shetani, na dhambi na mauti na katika Yeye tumefanywa zaidi ya kuwa washindi na twaweza kushinda na kupata taji la utukufu.

Nyota ya dhamiri yake imekuwa dhahiri na yenye kung'aa. Moyo wake umejawa na imani na Roho Mtakatifu. Malaika wa Mungu aliye juu yake, humkumbusha ahadi zenye thamani zitakazotolewa kwa wale walioshinda na kustahimili hata mwisho. (Ufunuo 2:7,11,17,26; 3:5,12,21). Mfuko wa fedha ulio wazi waonyesha kwamba si moyo wake tu, bali hata fedha zake na vyote alivyonavyo vimewekwa wakfu kwa Mungu. Badala ya kutumia mshahara wake kwa kufanya anasa za dhambi, huwasaidia maskini na humtolea Mungu fungu la kumi la vitu vyote anavyovipata, na zaidi ya haya hutoa sadaka nyingine kama awezavyo. Kwa kila njia hutumia fedha zake, kwa utukufu wa Mungu; kama ng'ombe amtoleavyo mwenye ng'ombe maziwa hali kadhalika Mkristo huyu, humtolea Mungu vitu vyake kwa moyo. Mzigo wa mikate na samaki waonyesha kwamba huishi maisha safi na ya kiasi Hatumii pombe wala divai, wala kujitia unajisi kwa kunywa damu, wala kula wanyama waliokufa wenyewe, wala kuvuta sigara kwa maana hukumbuka ya kwamba mwili wake unapaswa kuwa safi daima, kama hekalu la Mungu lilivyo. Moyo wake umekuwa nyumba ya sala, tena kwa kawaida hata katika jambo lolote, hakosi kuhudhuria mikutano ya Kanisa. Hupenda sala zifanywazo Kanisani na zile afanyazo mwenyewe ndani ya chumba chake. Huwakusanya jamaa zake kila siku na kuomba, kwa sababu anajua ya kwamba bila kuomba Mkristo, hawezi kuishi, atakuwa kama samaki ambaye hawezi kuishi bila maji. Kitabu kilichofunuliwa huonyesha kwamba, Biblia, yaani Neno la Mungu, ni kitabu kilichofunuliwa kwake, ambacho hukisoma na kukichunguza kwa bidii. Biblia ni taa ya miguu yake, tena ni upanga wake wa kupigania na kumshinda Ibilisi. Biblia ni mkate wake wa Kiroho, ambao hulisha roho yake siku kwa siku. Tena ni maji yanayotuliza kiu yake ya Kiroho. Mara kwa mara huoga mwili wake katika Neno la Mungu, tena hulitumia kama kioo cha moyo cha kujitazamia. Hupenda kuchukua msalaba ambao humkumbusha kuwa yeye mwenyewe amesulibiwa pamoja na Kristo tena amefufuka katika uzima mpya, kwa hiyo, anatafuta yale ya juu, yale ambayo ni ya milele, yale yasiyoonekana. Yu tayari kuonana na Mungu. Yu kama mti uliopandwa kando kando ya vijito vya maji, uzaao matunda yake kwa majira yake, tena amekuwa kama tawi la mzabibu wa kweli, ambalo huzaa matunda mengi. Upendo wa Mungu uliokamili umejazwa moyoni mwake, na kwa hiyo, haogopi mauti. (Zaburi 1:1-3; Yohana 15:1-14; Yohana 4:18-21).

## 10. PICHA YA KUMI

Yesu alisema, "Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima; yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi, naye kila aishiye na kuamini hatakufa kabisa hata milele." (Yohana 11:25,26). "Yeye alisikiaye Neno langu na kumwamini Yeye aliye nituma yuna uzima wa milele, wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani." (Yohana 5:24). Mauti haina hofu wala adhabu kwa Mkristo, kwa sababu mauti imemezwa na kushindwa. "Kuwapi, Ewe mauti kushinda

Copyright: ANGP

kwako? Uwapi, Ewe mauti uchungu wako? Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo." (1 Wakorintho 15:54-57).




Mtu anaye mcha Mungu, haogopi kufa. Kuondoka katika ulimwengu huu kutakapo fika, atakwenda zake kwa furaha kwenye nyumba iliyokamili na ya milele. Mtume Paulo alisema, "Ninatamani kwenda zangu nikakae na Kristo, maana ni vizuri zaidi sana." (Wafilipi 1:23). Mkristo huamini kuona uso wa Yesu, aliyemfia msalabani na aliyemkomboa kwa damu yake mwenyewe. Roho Mtakatifu humkumbusha maneno ya Yesu yanayosema, "Msifadhaike mioyoni mwenu, mnamwamini Mungu, niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi. Nitakuja tena, niwakaribishe kwangu, ili nilipo mimi nanyi muwepo." (Yohana 14:1-4). "Jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu, mambo ambayo Mungu amewaandalia wale wampendao." (1 Wakorintho 2:9). Ulimwenguni hakuna lugha inayofaa kueleza wala kuonyesha utukufu wa mahali pa mbinguni palipoandaliwa washindao hapaduniani na wamwaminio Yesu Kristo.

Katika picha hii ya kumi twakumbushwa juu ya kwenda kwake Mkristo mwaminifu wa kweli aliye ndani ya Kristo. Badala ya baba wa mauti, malaika wa Mungu huonekana. Anangoja kumrudishia Mungu Roho ambayo imehesabiwa haki. Nafsi na roho zimefunguliwa kutoka katika mwili, na zimepelekwa kwake aliyempenda. Kukaribishwa kwa furaha kunamngojea mbele za Mungu. Bwana humwambia,, "Vema, mtumwa mwema na mwaminifu, ingia katika furaha ya Bwana wako." (Matayo 25:21). Shetani hana nguvu tena juu yake, kwa sababu inathamani machoni pa Bwana mauti ya wacha Mungu wake. (Zaburi 116:15). Nikasikia sauti kutoka mbinguni ikisema, Andika, Heri wafu wafao katika Bwana tangu sasa: Naam, asema Roho, wapate kupumzika baada ya tabu zao; kwa kuwa matendo yao hufuatana nao. (Ufunuo 14:13).

Copy ... ANGP

Msomaji mpenzi usomaye kitabu hiki, Mungu akusaidie kumpa Yesu moyo wako kwa maana anasema, "Mwanangu, binti yangu, nipe moyo wako." Usiruhusu moyo wako mwerevu upate kupotea kwa kuzifuata tamaa za novu, kwa sababu mwenye kutumainia moyo wake ni mjinga. Uziache dhambi zako ukashike haki, kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.

Na wewe uliyempa Mungu maisha yako, shika kielezo cha maneno yenye uzaima, katika imani na upendo ulio katika Kristo Yesu, kwa maana wamjua yeye unayemuamini, na kusadiki ya kwamba aweza kulinda kile ulichokiweka amana kwake hata siku ile. Jejengeni juu ya imani yenu iliyo takatifu sana, ombeni katika Roho Mtakatifu, jilindeni katika upendo wa Mungu, mkimtazama Yesu, Mwenye kuanzisha na Mwenye kutimiza imani yetu, tena Mwenye kurudi upesi, aliye Mfalme wa wafalme.

Yeye awezaye kuwalinda ninyi msijikwae, na kuwasimamisha mbele ya utukufu wake bila mawaa katika furaha kuu. Yeye aliye Mungu pekee, Mwokozi wetu kwa Yesu Kristo Bwana wetu, utukufu una Yeye, na ukuu na uwezo, na nguvu, tangu milele, na sasa, na hata milele. Amini. (Yuda 24,25).

Twende mbele kwa jina lake
Hata aje Mwokozi yule,
Atatukaribisha kwake,
Tutawale naye milele.
Sauti zetu tuinue
Kumsifu Mwokozi yule,
Ili watu wote wajue
Wokovu u kwake milele,
Piga mbio, Twonane milele,
Twonane bandarini kule.

Copyright: ANGP

## A SPECIAL WORD FROM ANGP
## UN MONDE SPÉCIAL DE L'ANGP
## UMA PALAVRA ESPECIAL DA ANGP

**This booklet "The Heart of Man" is available in over 538 languages and dialects spoken throughout the world (Africa, Asia, The Far East, South America, Europe, etc.) Our Heart Book is now also available on cell phones, tablets, etc from www.angp-hb.co.za**

**Le livre du "Coeur de l'homme" peut etre obtenu en plus de 538 langues et dialectes parles dans le monde entier, a savoir: Afrique, Amerique, Asie, Extreme Orient, Europe. Notre Livre du Coeur est maintenant aussi disponible sur votre Telephone cellular, plaques, etc. de www.angp-hb.co.za**

**Este livro "O Coracao do Homem" e obtfdo em mais de 538 linguas e dialectos falados em todo o mundo, a saber: (Africa, Asia, America do Sul, Extremo Oriente, Europa, etc). O nosso Livro O Coração do Homem tambem esta agora disponivel em telefone celular, tablets, etc. de www.angp-hb.co.za**

**The 10 heart pictures contained in this booklet are also available in the form of large coloured picture charts (86 x 61cm) bound together in a set of 10 pictures. These "Heart Charts" can be obtained with European or African features and are particularly suitable to be used in conjunction with the Heart Book for class-teaching, open air evangelization etc. Kindly contact us to ascertain the latest subsidized price of this chart.**

**Les 10 images du coeur qui figurent dans ce livre peuvent etre obtenues en tableaux de couleur, format 86 x 61 cm, avec des physionomies europeennes ou africaines. Ils peuvent etre utilises en meme temps que le livre du coeur pour des classes bibliques, a l'ecole du dimanche ou lors de reunions de plein air. Soyez aimable de nous contacter pour assurer les derniers prix en cours du tableau.**

**As 10 imagens do coracao, contidas neste livro podem ser obtidas num conjunto de 10 imagens em colorido no tamanho de (86 x 61 cm). Estes "Cartazes do Coracao podem ser obtfdos com caracterfsticas Europeias e Africanas e podem ser usados em conjuncao com o mesmo livro em classes de ensino biblico, evangelizacao ou ao ar livre. Agradeciamos que nos contacta- se para confirmacao do ultimo preco dos cartazes.**



**Kindly write to us if you are able to assist us with further translations of our free Gospel literature, informing us of the language into which you could translate this Gospel literature. Your assistance would be appreciated.**

Copyright: ANGP

**If you have found salvation in Christ, or have been otherwise blessed through our Gospel literature, please let us know. We would like to thank God with you, and remember you further in our prayers.**

**Nous vous invitons a nous contacter pour faire des arrangements concernant de nouvelles traductions de notre litterature, nous informant de la langue dans laquelle vous pouvez traduire cette litterature evangelique. Votre aide sera beaucoup appreciee.**

**Si vous avez trouve le salut en Christ ou si vous avez ete beni par notre litterature, nous vous prions de nous le faire savoir. Nous aimerions remercier Dieu avec vous et prier pour vous.**

**Nos vos convidamos a nos contactar, afim de fazer qualquer arranjo concernente a novas traducoes de nossa literatura em outras Ifnguas. Vossa assistencia sera muito apreciavel.**

**Se tem encontrado a salvacao em Cristo, ou se tem sido abencoado por intermedio da nossa literatura evangelica, faca o favor de nos informar. Pois nos gostarfamos de agradecer a Deus juntamente convosco, e lembra-lo sempre em nossas oracoes.**

**For free Gospel literature, books and tracts in over 538 languages, write to:**

**Pour obtenir gratuitement de la litterature evangelique, des livres et des traites en plus de 538 langues, ecrivez a:**

**Para obter gratuftamente a literatura evangelica, livros e folhetos em mais de 538 Ifnguas diferentes escreva para:**

**ALL NATIONS GOSPEL PUBLISHERS**
**P.O. Box 2191**
**PRETORIA**
**0001**
**R.S.A.**

Copyright. ANGP

**A Gospel Literature Mission financed by donations**
**Une Mission de litterature evangelique financee de dons**
**Missao de literatura Evanqelica financiada por donativos**

**(Reg. No. 1961/001798/08)**